

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**

**Telegramu: "LEGAL"**

**Simu Na.: +255 26 2310019**

**Nukushi: +255 26 2310056**

**Barua Pepe: km@sheria.go.tz**

**DodomaTovuti: [www.sheria.go.tz](http://www.sheria.go.tz)**



Mji wa Serikali Mtumba,  
Mtaa wa Katiba,  
S. L. P. 315,  
**40484 DODOMA**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**TANZANIA KURINGIZA ZAIDI YA SHILINGI BILIONI 18 KUPITIA KIKAO CHA  
77 CHA TUME YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

**19 Oktoba, 2023 ARUSHA**

Kikao cha 77 cha Kawaida cha Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kitafanyika kwa takriban siku 20 katika Jiji la Arusha, ambapo masuala mbalimbali yatajadiliwa, yakiwemo maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu Afrika kwa kuzingatia Itifaki ya Maputo, Taarifa kuhusu Hali ya Haki za Binadamu Barani Afrika pamoja na Msaada wa Kisheria na Upatikanaji wa Haki katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Akielezea faida za kikao hicho kwa waandishi wa habari Jijini Arusha mapema leo, Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana alieleza kuwa Kikao hicho kitaiongezea sifa na heshima Tanzania kwani kitadhihirisha uwezo wa Tanzania katika kupokea na kuwahudumia wageni kwa huduma mbalimbali zikiwemo utalii, biashara, usafirishaji, malazi pamoja na uwekezaji.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Bi. Mary Makondo akimkaribisha Waziri kuongea na wanahabari alisema hii ni nafasi ya kipekee ambayo nchi yetu imepata na akatoa rai kwa wataanzania kuitumia fursa ya mkutano huu katika kujiendeleza kiuchumi kupitia ridhaa ya Rais Samia kuwa kikao hiki kifanyike nchini Tanzania.

Naye Mtendaji Mkuu wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC) Bw. Ephraim Mafuru alieleza kuwa AICC ni mwanachama wa AICA, ambacho ni chombo kinachofanya utafiti kuonesha faida za mikutano kama hii. Kwa idadi ya wageni ambao ni zaidi ya 900 waliojisajili hadi sasa kwenye mnyororo wa thamani ya utalii wa mikutano, Tanzania itaingiza zaidi ya shilingi za kitanzania Bilioni 18, kwani kwa wastani kila mgeni atatumia kiasi cha shilingi Milioni Moja kwa siku na hivyo kutoa fursa ya ongezeko la matumizi na kuingiza fedha za kigeni zitakazoleta matokeo chanya katika mawanda ya kiuchumi.

Lusajo Mwakabuku

**MKUU WA KITENGO CHA  
MAWASILIANO SERIKALINI**